**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO**
*(Barua zote zitumwe kwa Mkuu wa Shule )*

Tarehe 31/05/2023

MZAZI/MLEZI WA;… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … ..

S.L. P… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … …

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MALAMBO WILAYA YA NGORONGORO MKOA WA ARUSHA MWAKA 2023.**

## 1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2023 tahasusi ya CBG/HGL.Kuchaguliwa kwake ni kutokana na kufanya vizuri katika mtihani wake wa taifa kidato cha nne 2022.Shule ya sekondari Malambo ipo katika kijiji cha Malambo, Tarafa ya Sale,Wilaya ya Ngorongoro, Mkoa wa Arusha. Shule ipo katika mazingira mazuri na hali ya hewa nzuri ya mwanafunzi kusoma na kujisomea. Shule ya Sekondari Malambo ipo umbali wa km 96 kusini mwa mji mkuu wa halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro (LOLIONDO), km 140 kutoka Karatu upande wa Kaskazini. Kwa watakaotokea njia ya Arusha mjini hadi Karatu nauli ni shilingi 7000. Wanaotoka mikoa ya Mara na Simiyu wanaweza kutumia mgari ya yanayopita Serengeti na watashukia Karatu mjini. Watakaotokea Babati,Singida,Dodoma na Mwanza wanaweza kushukia Makuyuni na kupanda magari yanayokwenda Karatu mjini, Upo usafiri kutoka Dar-es-Salaam hadi Karatu kwa kutumia gari la Dar express. Kutokea Karatu kwenda Malambo upo usafiri wa uhakika siku ya Jumapili saa 12 kamili asubuhi kwa ghrama ya 20,000/= kwa mabasi ya Loliondo coach, hivyo ni vema ukafika siku ya Jumamosi ili kuamkia safari. Unashariwa kukata tiketi mapema, kwa mawasiliano zaidi piga 0754789696, 0787789696 Kwa wakala wa

basi ya Loliondo coach ofisi ya karatu.

Tunamkaribisha mwanao na kumtakia safari njema ya kuja Malambo.

**Mambo muhimu ya kuzingatia**

A. **Sare za shule**

a. Sare ya shule hii ni sketi mbili(2) nyeusi kitambaa kizito ,zenye marinda ya kawaida zinazofika kwenye kisigino

(marinda 8) pamoja na mashati mawili (2)meupe mikono mirefu.

b. Kwa waislam rangi ya kijuba iwe na rangi nyeupe

c. Nguo za kushindia(shamba dress) sketi mbili ya rangi ya ugoro kitambaa kizito cha suti marinda ya kawaida zinazofika kwenye kisigino.

d. T- shirt za dark blue colar nyeupe na michirizi yenye rangi ya dark blue shingoni,mikono rangi nyeupe na michirizi dark blue.,isiyo na maandishi yenye nembo ya shule (zinapatikana shuleni kwa gharama ya elfu kumi na mbili).

e. T-shirt ya michezo ya kijani yenye nembo ya shule. (zinapatikana shuleni kwa gharama ya shilingi elfu kumi na mbili)

f. Sweta jozi moja rangi nyeusi yenye V

g. Tracksuit rangi nyekundu pea 1

h. Chandarua 1kwa ajili ya kujikinga na mbu

i. Soksi jozi mbili ndefu, nyeupe zisizo na alama yeyote

j. Rangi ya viatu, nyeusi yenye mkanda moja (Juma na Rosa).

B. **Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anatakiwa kuleta shuleni**

a. Madaftari makubwa(counterbooks) yasiyopungua kumi

b. Kalamu ,rula na ufutio

c. Tochi moja inayotumia mwanga wa jua kwa matumizi binafsi.

d. Kikokotozi/ Scientific calculator na dissecting kit kwa tahasusi ya CBG

e. Godoro futi $2\frac{1}{2}$

f. Blanketi moja

g. Ndoo ya plastiki lita 10 ya matumizi binafsi

h. Vyombo vya chakula kama sahani, kikombe, bakuli na kijiko vyote ni vya bati,na kidumu cha kutunzia maji ya kunywa

i. Taulo ya kuogea

j. Shuka za blue bahari jozi/pea mbili (mashuka ya kimasai hayaruhusiwi)

k. Aje na vitabu kwa matumizi binafsi kulingana na tahasusi (combination

l. Rimu ya karatasi mbili (A4 aina ya DOUBLE A) kwa mwaka mzima kwa ajili ya mazoezi mbalimbali

m. Vifaa vya usafi –chelewa ,ufagio wa ndani(soft broom),Hard broom, squeezer

n. File la plastik 1

**2.0 Sheria na kanuni Muhimu za Shule hii.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu sayansi na teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais–TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

2.1 Heshima kwa viongozi , wazazi ,wafanyakazi wote ,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

2.2 Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

2.3 Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (night preparation)

2.4 Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

2.5 Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika

shule hii.

2.6 Kutunza usafi wa mwili ,mavazi na mazingira ya shule

2.7 Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa

2.8 Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, na

2.9 Kutunza mali za umma.

**NB**: 1.Mshauri binti yako asome sheria za shule kwa makini na kuzielewa.

2.Mshauri kuzingatia masomo zaidi ili aweze kufaulu na kujiunga na elimu ya juu

3.Vipodozi ,pafyumu,redio,kamera,simu pamoja na nguo za nyumbani

haviruhusiwi shuleni,ukaguzi utafanyika kabla ya kuingia bwenini na piah utafanyika

ukaguzi wa dharura akikutwa navyo bwenini hatua za kinidhamu zitachukuliwa .

4. Hakikisha binti yako ajapo shuleni amepima afya kikamilifu na kama anachangamoto yeyote kiafya ni vyema kuleta taarifa zake kuwasilisha shuleni ili aweze kupata usaidizi pale changamoto itakapojitokeza.

3. **Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au Kusimamishwa shule**

2.1 Wizi

2.2 Utoro wa zaidi ya siku 90

2.3 Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu,walezi na jamii kwa ujumla.

2.4 Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule.

2.5 Uasherati

2.6 Ubakaji

2.7 Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine , mirungi, kubeli, sigara, ugoro na kadhalika.

2.8 Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

2.9 Kudharau Bendera ya Taifa

2.10 Kuoa au kuolewa

2.11 Kutoa mimba

2.12 Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

2.13 Kukataa adhabu kwa makusudi

2.14 Kuwa na simu ya mkononi.

**3.0 Mambo Mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**

3.1 Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

3.2 Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo ,fujo, na makosa ya jinai.

3.3 Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**4.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo /maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

… … … … … … … … … … … … … … … … … … … …
**Aziz Amran Kaduma**
**MKUU WA SHULE**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A**

To The Medical Officer
…………………………………………………………
…………………………………………………………
…………………………………………………………
Mr. & Mrs./Miss…………………………………………………

Please examine the above name as to his/her fitness mentally and for a full time secondary Education. The examination should include the following categories (i-iii) each category or sub-category of which will render the applicant ineligible in case of any defects.
Pregnancy (category iv) will also render a girl candidate in eligible for the secondary Education.

i. (a) Eye-sight
   (b) Hearing
   (c) Limbs
   (d) Speech
   ( e) Venereal Diseases
   (f) Leprosy
   (g) Epilepsy
ii. Neuroses
iii. Other serious diseases
iv. Pregnancy

**DATE…………………………………………………………SIGANATURE…………………………………**

**PART B**

I have examined the above named and consider that he/she is fit/unfit for full time Secondary Education.

i.
a) Eye-sight…………………………………………………………
b) Hearing…………………………………………………………
c) Limbs…………………………………………………………
d) Speech…………………………………………………………
e) Venereal Diseases…………………………………………
f) Leprosy…………………………………………………………
g) Epilepsy…………………………………………………………
ii. Neuroses…………………………………………………………
iii. Other serious diseases……………………………………
iv. Pregnancy…………………………………………………………

**DATE……………………………SIGNATURE……………………DESIGNATION………………..**

**OFISI YA RAISI-TAMISEMI**
**SHULE YA SEKONDARI MALAMBO S.L.P 46 LOLIONDO**

**TAARIFA YA MKATABA WA UTII KWA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI**

## 1. TAARIFA (HISTORIA ) YA MWANAFUNZI

1.1 Jina la mwanafunzi
… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … …
Jinsi (me/ke)… … … … … … … .umri… … … … … … … … … … .
Mtaa/ Kijiji anapoishi… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … …

1.2 Jina la Mzazi/Mlezi… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … ..
Mji/kijiji/mtaa anapoishi
… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … …
Mawasiriano ya mzazi/mlezi. Simu ya mkononi , Baba /mama… … … … … … … … … … … … …

## 2. MKATABA WA KUTO SHIRIKI MIGOMO,FUJO NA MAKOSA YA JINAI SHULENI

Mimi … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … ..naahidi kwamba sitashiriki migomo ya aina yeyote shuleni, sitafanya fujo zozote shuleni wala kutenda kosa lolote la jinai na nakubali kutii sheria, kanuni na taratibu na maelekezo yote nitakayopewa katika muda wote nitakapo kuwa shuleni.

Jina la mwanafunzi:… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … …
Sahihi: … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … .
Tarehe:… … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … …

## 3. KUKIRI KWA MZAZI KUTOA USHIRIKIANO

Mimi … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … ambaye ni mzazi/mlezi wa … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … nakiri kukubaliana na sheria na kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule wakati wote atakapokuwa anasoma

Jina … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … …
Sahihi … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … .
Tarehe … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … … ..

**MUHIMU**; *Fomu hii ijazwe na kurudishwa shuleni*